# RIPOTI YA UWEKEZAJI TANZANIA 2025

## UWEKEZAJI WA MITAJI BINAFSI KUTOKA NJE

# MUHTASARI

# RIPOTI YA UWEKEZAJI TANZANIA 2025

## UWEKEZAJI WA MITAJI BINAFSI KUTOKA NJE

# MUHTASARI

# UTANGULIZI

Ripoti ya Uwekezaji Tanzania ya mwaka 2025 inachambua kwa kina mwenendo wa mitaji binafsi kutoka nje iliyoingia nchini kupitia aina mbalimbali za uwekezaji. Uchambuzi huu unahusisha uwekezaji wa moja kwa moja unaojumuisha umiliki wa hisa kuanzia asilimia 10 na zaidi (*Foreign Direct Investment – FDI*), uwekezaji wa hisa chini ya asilimia 10 (*Portfolio Investment – PI*), pamoja na uwekezaji mwingine unaotokana na uwekezaji kwa wasio wanahisa katika makampuni yaliyowekeza nchini (*Other Investment – OI*). Ripoti inaonesha kuwa, licha ya changamoto zinazoendelea katika uchumi wa dunia, ikiwemo migogoro ya kibiashara na hali ya kutotabirika kwa sera za kiuchumi, uchumi wa Tanzania umeendelea kuwa imara, sambamba na kuimarika kwa mazingira ya kiuchumi, kupelekea kuchagiza shughuli za uwekezaji.

Hivyo basi ripoti hii inachambua vyanzo vikuu vya mitaji binafsi kutoka nje, mwenendo wa uwekezaji kwa kipindi husika, pamoja na mgawanyo wa uwekezaji kwa mujibu wa sekta za kiuchumi. Uchambuzi huu unalenga kutoa mwelekeo halisi wa mchango wa uwekezaji wa kigeni katika kuimarisha shughuli za uzalishaji, ajira na ukuaji wa uchumi kwa ujumla.

Ripoti hii imeandaliwa kwa ushirikiano wa taasisi tatu za Serikali ambazo ni Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi Tanzania (TISEZA), pamoja na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS). Mchakato wa uandaaji wa ripoti ulisimamiwa kupitia mfumo wa ngazi kuu tatu, unaojumuisha Kamati ya Wakuu wa Taasisi

(Executive Committee), Kamati ya Uongozi (Steering Committee), na Kamati ya Wataalamu (Technical Committee). Kamati ya Wataalamu ndio ilitekeleza shughuli za ukusanyaji wa takwimu, uchambuzi na uandaaji wa ripoti.

Kwa ujumla, ripoti inalenga kuonesha mchango wa uwekezaji wa mitaji binafsi kutoka nje katika uchumi wa Tanzania na kutoa taarifa zitakazotumika katika upangaji wa sera na mikakati ya kukuza uwekezaji. Madhumuni mahsusi ya ripoti hii ni pamoja na:

- Kuchambua na kuimarisha takwimu za uwekezaji wa mitaji binafsi kutoka nje kwa ajili ya matumizi katika mizania ya urari wa malipo na tathmini ya nafasi ya uwekezaji wa kimataifa nchini;
- Kutoa mapendekezo ya sera na mikakati ya kuendeleza mazingira bora ya biashara na uwekezaji; na
- Kubainisha fursa za uwekezaji zilizopo nchini kwa lengo la kuvutia mitaji ya ndani na ya kigeni.

Ripoti hii inawasilisha muhtasari wa matokeo muhimu yaliyotokana na utafiti wa uwekezaji wa mitaji binafsi kutoka nje kwa mwaka 2024. Utafiti huu ulihusisha makampuni yaliyochaguliwa kwa kuzingatia vigezo vya kitakwimu (sampuli), ambapo jumla ya makampuni 563 yenye uwekezaji wa kigeni yalihusishwa, na kiwango cha mwitikio kilifikia asilimia 86.

Ripoti kamili (*Tanzania Investment Report 2025*) inapatikana katika tovuti za Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi Tanzania (TISEZA), na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS).

# MATOKEO MUHIMU

## Uwekezaji wa Mitaji Binafsi Kutoka Nje

Mwaka 2024, uwekezaji wa mitaji binafsi kutoka nje uliendelea kuongezeka, ukiashiria kuimarika kwa imani ya wawekezaji wa kigeni katika uchumi wa Tanzania. Thamani ya limbikizo (*stocks*) la uwekezaji wa mitaji binafsi kutoka nje liliongezeka kwa asilimia 12.1 na kufikia dola za Marekani milioni 24,754.1 (Jedwali 1). Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (FDI), uliokuwa na mchango wa asilimia 87.7 ya jumla ya uwekezaji, huku uwekezaji mwingine (OI) ukichangia asilimia 11.2. Ongezeko hili linaashiria kuendelea kuimarika kwa mazingira mazuri ya uwekezaji, yanayochangiwa na uthabiti wa uchumi, sera madhubuti za uwekezaji na maboresho ya miundombinu ya uzalishaji na biashara.

### Jedwali 1: Uwekezaji wa Mitaji Binafsi Kutoka Nje

Dola za Marekani Milioni


| Aina | Uingiaji | | | | | Limbikizo | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
| Uwekezaji wa moja kwa moja | 943.8 | 1,190.5 | 1,437.6 | 1,648.9 | 1,656.0 | 15,612.6 | 15,741.1 | 18,095.8 | 19,455.3 | 21,698.9 |
| Hisa na Uwekezaji wa wanahisa | 903.0 | 961.6 | 1,312.3 | 938.4 | 1,398.3 | 9,548.6 | 10,201.0 | 9,899.3 | 10,673.2 | 12,652.7 |
| Hisa na Uwekeza wa Wanahisa isipokuwa mapato ya faida | 327.0 | 392.5 | 492.3 | 213.5 | 290.6 | 9,368.2 | 5,807.4 | 6,399.4 | 6,965.6 | 7,595.1 |
| Uwekezaji wa Mapato ya Faida | 576.0 | 569.1 | 820.0 | 724.9 | 1,107.7 | 180.4 | 4,393.6 | 3,499.9 | 3,707.5 | 5,057.6 |
| Mikopo | 40.8 | 228.9 | 125.3 | 710.5 | 257.7 | 6,064.0 | 5,540.1 | 8,196.4 | 8,782.2 | 9,046.3 |
| ya muda mrefu | 94.6 | 173.7 | -25.1 | 558.9 | 203.9 | 5,581.6 | 5,196.1 | 6,294.5 | 7,698.1 | 7,986.6 |
| ya muda mfupi | -53.9 | 55.2 | 150.4 | 151.6 | 53.9 | 482.3 | 343.9 | 1,902.0 | 1,084.1 | 1,059.7 |
| Uwekezaji mdogo wa moja kwa moja | 1.8 | 4.9 | 0.2 | 1.4 | 6.5 | 124.8 | 126.8 | 195.8 | 216.7 | 272.7 |
| Uwekezaji mwingine | -85.5 | -8.6 | 308.1 | 44.5 | 322.1 | 2,724.5 | 3,056.5 | 3,890.8 | 2,402.4 | 2,782.5 |
| Mikopo ya muda mrefu | -32.7 | -12.9 | 190.3 | -142.2 | 51.8 | 2,127.4 | 2,236.9 | 2,730.5 | 1,564.8 | 1,668.0 |
| Mikopo ya muda mfupi | -3.0 | -15.5 | 0.4 | -47.9 | 8.7 | 50.9 | 185.8 | 154.3 | 363.3 | 339.9 |
| Biashara malipo ya awali | -47.4 | 16.5 | 117.1 | 234.4 | 257.7 | 301.5 | 610.3 | 996.5 | 405.3 | 695.3 |
| Amana na sarafu | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Hisa nyinginezo | -2.5 | 3.3 | 0.3 | 0.2 | 3.9 | 244.7 | 23.5 | 9.4 | 68.9 | 79.3 |
| Jumla ya Uwekezaji Binafsi wa Kigeni | 860.1 | 1,186.8 | 1,745.8 | 1,694.8 | 1,984.6 | 18,461.9 | 18,924.3 | 22,182.4 | 22,074.4 | 24,754.1 |

*Maelezo: Uwekezaji Mwingine (OI) unahusisha aina yoyote ya uwekezaji ambao haujajumuishwa ndani ya Uwekezaji wa moja kwa moja (FDI) na Uwekezaji wa Hisa (PI).*

## 1. Uwekezaji wa Moja kwa Moja Kutoka Nje (FDI)

**Kielelezo1: Uwekezaji wa Moja kwa Moja (FDI)**

Dola za Marekani Milioni





Uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (FDI) unaendelea kuwa kichocheo kikuu cha ukuzaji mitaji na maendeleo ya sekta binafsi nchini. Mwaka 2024, uwekezaji huu ulifikia dola za Marekani milioni 1,656, sawa na ongezeko la asilimia 0.4 kutoka dola za Marekani milioni 1,648.9 mwaka 2023 (Kielelezo 1). Ingawa ongezeko ni la kiwango cha chini, linadhihirisha ustahimilivu wa uchumi wa Tanzania katika kipindi ambacho masoko ya fedha duniani yamekuwa na masharti magumu, pamoja na hali ya kutotabirika kwa sera za kiuchumi duniani. Kwa muktadha wa kimataifa, shughuli za kiuchumi Tanzania zimeendelea kuimarika, sambamba na juhudi za serikali za kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

## 1.1 Ufadhili wa Uwekezaji wa Moja kwa Moja Kutoka Nje (FDI)

**Kielelezo 2: Vyanzo nya mitaji ya FDI**

Asilimia





Ufadhili wa FDI mwaka 2024 ulionesha mabadiliko yanayoelekea zaidi kwenye vyanzo vya ndani vya makampuni yaliyowekeza nchini, jambo linaloashiria kuimarika kwa faida na uwezo wa makampuni kubaki na mapato kwa ajili ya ukuzaji wa biashara. Tofauti na mwaka 2023 ambapo mikopo kati ya makampuni yanayohusiana (*related companies*) ilichangia zaidi, wakati kwa mwaka 2024 faida zilizorejeshwa katika biashara ziliongezeka zaidi na kufikia dola za Marekani milioni 1,107.7 kutoka dola za Marekani milioni 724.9 (Kielelezo 2). Wakati huohuo, mikopo kutoka kwa makampuni yanayohusiana ilishuka hadi dola za Marekani milioni 257.7, kutokana na kupungua kwa mikopo mipya pamoja na urejeshwaji mkubwa wa mikopo iliyotolewa miaka iliyopita. Hali hii inaakisi mazingira mazuri na wezeshi ya uwekezaji, ambapo faida zinazopatikana na uwekezaji zinarejeshwa kwenye biashara ili kuendelea kuchagiza ukuaji wa biashara.

## 1.2 Shughuli za Kiuchumi Zilizoongoza katika Uwekezaji wa Moja kwa Moja

Kwa mwaka 2024, Uwekezaji wa Moja kwa Moja katika shughuli za kiuchumi unaonesha kuendelea kujikita kwenye shughuli chache, hususan: uchimbaji madini na uchorongaji (dola za Marekani milioni 442.2), fedha na bima (dola za Marekani milioni 401.3), uzalishaji bidhaa viwandani (dola za Marekani milioni 223.1), pamoja na habari na mawasiliano (dola za Marekani milioni 152.1). Kwa pamoja, shughuli hizi zilichangia zaidi ya asilimia 73 ya uwekezaji wote (Kielelezo 3). Aidha, kumekuwa na ongezeko la mchango wa shughuli za kilimo, ujenzi, usafirishaji na uhifadhi, pamoja na biashara ya jumla na rejareja. Hali hii inaashiria mwelekeo chanya wa kupanuka kwa wigo wa shughuli zinazovutia uwekezaji wa moja kwa moja.

**Kielelezo 3: Shughuli zenye mchango mkubwa kwenye FDI**


Asilimia



Baadhi ya shughuli zilionesha ongezeko kubwa ikilinganishwa na mwaka uliotangulia, hususan kilimo, ujenzi, fedha na bima, na usafirishaji na uhifadhi. Shughuli za fedha na bima zilirekodi ongezeko kubwa zaidi, ambapo uwekezaji uliongezeka kwa asilimia 50 na kufikia dola za Marekani milioni 401.3, ukichangiwa na upanuzi wa huduma za kifedha za kidijitali kwa njia ya simu na benki, na maboresho ya mifumo ya udhibiti yaliyoimarisha uwazi na ujumuishi wa kifedha. Kadhalika, uwekezaji katika kilimo, misitu na uvuvi uliongezeka zaidi ya mara mbili hadi dola za Marekani milioni 130.4, ukionesha kuimarika kwa imani ya wawekezaji kwenye kilimo na uongezaji thamani. Shughuli za ujenzi, na usafirishaji na uhifadhi nazo zilivutia dola za Marekani milioni 112.9 na 77.4 mtawalia, zikichangiwa zaidi na utekelezaji wa miradi mikubwa ya miundombinu, ikiwemo upanuzi wa bandari nchini, Reli ya Kisasa (SGR) kwenye njia ya Dar es Salaam – Dodoma, na maendeleo ya mfumo wa Mabasi yaendayo Haraka (BRT) jijini Dar es Salaam (Kielelezo 4).

**Kielelezo 4: Shughuli zilizoonesha ongezeko kubwa kwa Mwaka 2024**


Dola za Marekani Milioni



Licha ya mwenendo huo, uchimbaji madini na uchorongaji pamoja na uzalishaji bidhaa viwandani viliendelea kuwa na mchango mkubwa, ingawa zilipungua ukilinganisha na mwaka 2024. Uwekezaji kwenye madini ulifikia dola za Marekani milioni 442.2, ukipungua kutokana na ulipaji wa mikopo kati ya makampuni na hasara zilizopatikana kwa baadhi ya kampuni zilizo kwenye hatua za awali za utafiti wa madini (exploration). Hata hivyo, limbikizo la uwekezaji wa moja kwa moja kwenye madini lilifikia dola za Marekani milioni 9,798.7 mwaka 2024, sawa na asilimia 45.2 ya limbikizo lote la uwekezaji wa moja kwa moja. Kwa upande wa uzalishaji viwandani, uwekezaji wa moja kwa moja ulifikia dola za Marekani milioni 223.1 mwaka 2024, ikiwa ni chini ya dola za Marekani milioni 364 mwaka 2023, ikichangiwa zaidi na ulipaji wa mikopo ya kati ya makampuni; hata hivyo, limbikizo lilibaki imara na kufikia dola za Marekani milioni 3,344.9, sawa na asilimia 15.4 ya limbikizo lote (Kielelezo 5), likiakisi jitihada za serikali katika kuendeleza sera ya viwanda.

**Kielelezo 5: Uwekezaji wa Moja kwa Moja kwa Shughuli Kuu**

Dola za Marekani Milioni




Shughuli nyingine kama habari na mawasiliano ziliendelea kufaidika na mahitaji ya huduma za kidijitali, huku biashara, umeme na gesi, mali isiyohamishika, na huduma za malazi na chakula zikikua kwa kasi ndogo. Aidha, uwekezaji wa moja kwa moja uliendelea kuwa mdogo katika shughuli zinazohusiana na elimu, afya na utafiti wa kisayansi. Shughuli hizi za kijamii zina uwezo mkubwa wa kuvutia uwekezaji, endapo tu kutakuwa na vivutio mahsusi (incentives) na uwepo wa mifumo ya upatikanaji wa mitaji iliyojengeka katika ufadhili mchanganyiko (blended finance) ili kuongeza mvuto kwa wawekezaji.

## 1.1 Nchi Chache Ziliendelea Kuongoza katika Uwekezaji wa Moja kwa Moja

**Kielelezo 6: Nchi Kumi Zinazoongoza kwa Uingiaji wa FDI**


Dola za Marekani Milioni



Mwaka 2024, nchi kumi zilizoongoza kwa FDI ziliendelea kuchangia sehemu kubwa ya uwekezaji, sawa na asilimia 64.7 ya FDI yote. Uingereza iliongoza kwa kuingiza dola za Marekani milioni 499.8, ikifuatiwa na Afrika Kusini, Falme za Kiarabu (UAE), na China (Kielelezo 6). Hali hii ilichangiwa zaidi na makampuni, faida za kisekta, na upanuzi wa biashara wa kimkakati hususan katika sekta za madini, fedha na bima, usafirishaji na uhifadhi, viwanda vya uzalishaji, pamoja na habari na mawasiliano. Aidha, kuongoza kwa Uingereza kunatokana na ununuzi wa hisa zilizokuwa zinamilikiwa na wanahisa kutoka Canada na Visiwa vya Cayman katika sekta ya madini. Vilevile, Mauritius imekuwa ikiongoza katika kuleta mitaji kwa ajili ya uwekezaji isipokuwa kwa mwaka 2024, hali hii ilichangiwa zaidi na kiwango kikubwa cha urejeshaji mikopo; na haimaanishi kuwa nia ya uwekezaji imepungua.

**Kielelezo 7: Nchi Kumi Zinazoongoza kwa limbikizo la FDI**

Dola za Marekani Milioni



Kwa upande wa limbikizo, Uingereza iliendelea kuongoza kwa umiliki wa asilimia 26.9 ya limbikizo lote la FDI mwaka 2024, ikifuatiwa na Mauritius pamoja na Norway (Kielelezo 7). Hali hii inaonesha kuwa Tanzania ina wigo mpana wa vyanzo vya mitaji ya kigeni, unaojumuisha nchi zilizokuwepo na zile zinazoibukia, na hivyo kuchagiza uwekezaji wa muda mrefu unaoelekezwa kwenye shughuli zenye mchango mkubwa kwa maendeleo.

## 2. Uwekezaji Mdogo Kutoka Nje (PI)

Uwekezaji mdogo (hisa) kutoka nje (PI) uliongezeka mwaka 2024 na kufikia dola za Marekani milioni 6.5 kutoka dola za Marekani milioni 1.4 mwaka 2023 (Jedwali 1). Ongezeko hili linaonesha kuongezeka kwa ushiriki wa wawekezaji wa kigeni katika masoko ya mitaji nchini, sambamba na kuimarika kwa viashiria vya soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE). Katika mwaka 2024, thamani ya soko la Hisa la Dar es Salaam iliongezeka hadi dola za Marekani bilioni 6.9 kutoka dola za Marekani bilioni 6.1 mwaka 2023 na Fahirisi ya Jumla ya Hisa (DSE All Share Index) kupanda kwa asilimia 22.2 kutoka kwenye punguzo la asilimia 7 mwaka uliopita. Uthabiti wa mauzo na manunuzi ya hisa, pamoja na shughuli za biashara katika dhamana za serikali na makampuni, vinaangazia juhudi za serikali katika kuimarisha masoko ya mitaji, huku uwekezaji wa hisa ukiendelea kuwa eneo lenye fursa kubwa ya kukua kama sehemu muhimu kwenye uwekezaji wa mitaji binafsi kutoka nje.

## 3. Uwekezaji Mwingine (OI)

Uwekezaji mwingine (OI), unaojumuisha zaidi madeni kutoka kwa wanahisa wasio na uhusiano (*unrelated parties*), ulirekodi faida kubwa mwaka 2024 na kufikia dola za Marekani milioni 322.1 kutoka dola za Marekani milioni 44.5 mwaka 2023. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na

mikopo ya kibiashara ya muda mfupi (trade credits) iliyofikia dola za Marekani milioni 257.7, ikiashiria kuimarika kwa mahusiano ya kibiashara nje ya mipaka (Jedwali 2). Uwekezaji huu ulielekezwa zaidi kwenye uchimbaji madini na uchorongaji pamoja na fedha na bima.

**Jedwali 2: Uwekezaji Mwingine**

Dola za Marekani Milioni


| | Uingiaji | | | | | Limbikizo | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
| Mikopo | -35.6 | -28.4 | 190.7 | -190.1 | 60.5 | 2,178.3 | 2,422.7 | 2,611.6 | 1,928.1 | 2,007.9 |
| ya muda mrefu | -32.7 | -12.9 | 190.3 | -142.2 | 51.8 | 2,127.4 | 2,236.9 | 2,730.5 | 1,564.8 | 1,668.0 |
| ya muda mfupi | -3.0 | -15.5 | 0.4 | -47.9 | 8.7 | 50.9 | 185.8 | 154.3 | 363.3 | 339.9 |
| Mikopo ya kibiashara na malipo ya awali | -47.4 | 16.5 | 117.1 | 234.4 | 257.7 | 301.5 | 610.3 | 996.5 | 405.3 | 695.3 |
| Hisa nyinginezo | -2.5 | 3.3 | 0.3 | 0.2 | 3.9 | 244.7 | 23.5 | 9.4 | 68.9 | 79.3 |
| Uwekezaji mwingine | -85.5 | -8.6 | 308.1 | 44.5 | 322.1 | 2,724.5 | 3,056.5 | 3,890.8 | 2,402.4 | 2,782.5 |

## 4. Faida baada ya kodi iliongezeka

Faida iliyopatikana baada ya kodi iliongezeka hadi dola za Marekani milioni 2,182.4 mwaka 2024 kutoka dola za Marekani milioni 1,806.3 mwaka 2023 (Kielelezo 8). Pamoja na ongezeko hilo, gawio lilishuka kwa asilimia 27.7 hadi dola za Marekani milioni 495.9, na kupelekea kuongeza kwa mapato yanayobaki ndani ya biashara. Aidha, faida iliyowekezwa nchini iliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 1,686.5, ikiendelea kuashiria imani kubwa waliyonayo wawekezaji katika uchumi wetu na dhamira ya kuendelea kuwekeza nchini. Faida ilipatikana zaidi kwenye shughuli za fedha na bima (dola za Marekani milioni 851), uchimbaji madini na uchorongaji (dola za Marekani milioni 648.9), na uzalishaji bidhaa viwandani (dola za Marekani milioni 292.7). Mwenendo huu unaimarisha nafasi ya mitaji inayozalishwa ndani ya nchi kama kichocheo muhimu cha uendelevu wa uwekezaji wa kigeni (Kielelezo 8).

## Kielelezo 8: Faida na Gawio

Dola za Marekani Milioni



# MWELEKEO WA UWEKEZAJI TANZANIA

## Mazingira ya Kiuchumi

Mwaka 2025, mazingira ya uchumi jumla yanatarajiwa kubaki thabiti, yakitegemezwa na utekelezaji wa mageuzi ya kiuchumi, kuimarika kwa miundombinu, na kurejea kwa nguvu kwa baadhi ya sekta za uzalishaji. Pato la Taifa linakadiriwa kukua kwa asilimia 5.9, likiongozwa na shughuli za kilimo, ujenzi na habari. Miradi ya usafirishaji na nishati inaendelea kuwa chachu ya ufanisi wa uzalishaji na biashara, hususan kupitia kuimarika kwa matumizi ya Reli ya Kisasa (SGR) na kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme wa Mradi wa Julius Nyerere—vinavyotarajiwa kupunguza gharama za usafiri, kuongeza ufanisi wa usafirishaji wa mizigo, kuimarisha uhusiano wa kikanda na minyororo ya thamani ya ndani.

Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kuwa ndani ya lengo la nchi la kati ya asilimia 3 hadi 5. Hali hii itachangiwa na upatikanaji wa chakula, ufanisi wa usafirishaji, uthabiti wa bei za bidhaa duniani hususan mafuta ghafi, na umadhubuthi wa sera za fedha na bajeti. Uthabiti wa kiwango cha ubadilishaji fedha za kigeni, pamoja na kuimarika kwa sekta ya nje, vinatarajiwa kuendelea kuunga mkono imani ya wawekezaji.

## Mikakati ya Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji

Kuimarisha mazingira ya uwekezaji nchini Tanzania ni muhimu ili kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2050, inayolenga kujenga uchumi shindani, jumuishi na endelevu. Aidha, Serikali inaendelea na jitihada za kuboresha mazingira ya uwekezaji, ikiwemo:

i. Kuongeza ufanisi wa huduma kwa wawekezaji kupitia Vituo vya Huduma Mahali Pamoja (One-Stop Facilitation Centre) na viwango vya uwazi katika utoaji huduma;
ii. Kuimarisha mfumo wa kisheria na kanuni kwa kuoanisha majukumu baina ya Taasisi;
iii. Kuendeleza majadiliano na ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi kwa ajili ya kutatua changamoto na kuhamasisha fursa;
iv. Kuongeza matumizi ya mifumo ya kidijitali kwenye huduma za serikali na mifumo ya malipo ili kupunguza gharama za miamala na kuchochea ubunifu;
v. Kuimarisha uratibu wa taasisi na uthabiti wa sera ili kusaidia mipango ya uwekezaji wa muda mrefu; na
vi. Kuendelea kuimarisha minyororo ya thamani ya kilimo kupitia pembejeo bora, umwagiliaji, huduma za ugani, na kuongeza wigo wa mikopo ya kilimo.

# HITIMISHO

Ripoti ya Uwekezaji Tanzania 2025 inaonesha kuendelea kwa mwelekeo chanya wa uwekezaji wa mitaji binafsi kutoka nje, ukichangiwa na uthabiti wa uchumi jumla, maboresho ya mazingira ya biashara na uwekezaji, na fursa zinazoendelea kupanuka katika sekta mbalimbali. Mwaka 2024, uwekezaji wa moja kwa moja uliendelea kuimarika (dola za Marekani milioni 1,656), huku vyanzo vya uwekezaji vikijikita vikielekea zaidi kwenye faida zilizorejeshwa, jambo linaloashiria kuimarika kwa faida na imani ya wawekezaji katika uchumi wetu. Aidha, uwekezaji wa hisa uliongezeka na kuonesha mwamko mpya kwenye masoko ya mitaji, wakati uwekezaji mwingine uliongezeka ukichangiwa na mikopo ya kibiashara.

Katika kipindi kijacho, juhudi za kuimarisha mazingira ya uwekezaji zitaendelea kuelekezwa kwenye kuboresha huduma kwa wawekezaji, kuharakisha mageuzi ya kidijitali, kuimarisha uratibu wa taasisi, kudumisha uwazi na uthabiti wa sera, pamoja na kuendeleza majadiliano ya mara kwa mara kati ya serikali na sekta binafsi. Hatua hizi zinaiweka Tanzania katika nafasi nzuri ya kuvutia uwekezaji wenye tija zaidi, kupanua msingi wa uzalishaji, kuimarisha ushindani wa mauzo ya nje, na kuharakisha kufikia malengo ya maendeleo ya muda mrefu.









**KWA MAELEZO ZAIDI, TAFADHALI TEMBELEA TOVUTI ZETU**

| TISEZA | BOT | NBS |
| --- | --- | --- |
| www.tiseza.go.tz | www.bot.go.tz | www.nbs.go.tz |